# UANZISHAJI WA KITALU CHA MICHE YA MIKOROSHO



**Kimetayarishwa na;**

Taasisi ya Utafit wa Kilimo Tanzania
TARI - Naliendele
S.L.B 509
MTWARA
Email: cdnaliendele@tari.go.tz

April 2019

**Kuandaa na kujaza mchanganyo wa udongo kwenye viriba**

Viriba vinaweza kutengenezwa kwa kutumia mifuko/karatasi ya plastiki;


Kiuchumi: viriba vidogo (i.e. sm 7.5 kipenyo, sm 20 kimo) vina manufaa zaidi kwa sababu huhitaji udongo kidogo na huchukua eneo dogo la kitalu kuliko viriba vikubwa.




1.Kata viriba katika urefu wa sentimeta 20.

2.Jaza mchanganyiko wa udongo kwenye viriba kwa kujaza ¼ hadi 1/3 ya kitako cha kiriba. Shindilia iwe ngumu kiasi cha kutoruhusu udongo kumwagika.

3.Kamilisha kujaza sehemu iliyobaki juu. Hakikisha viriba havina mikunjo baada ya kujaza.



*Ukataji na ujazaji udongo kwenye viriba*

4.Panga viriba juu ya karatasi ya nailoni kwa mstari vikiwa vimebanana kwenye kivuli. Karatasi ya nailoni huzuia mizizi isipenye kwenye ardhi. Viriba vinapangwa kwa kubananishwa ili kupunguza upotevu wa maji, kuanguka na kuharibika. Egeshea udongo kwenye mstari wa nje wa viriba ili kuhakikisha havianguki

**Uoteshaji wa mbegu kwenye kiriba.**

1. Panda moja kwa moja kwenye viriba kama upo uhakika wa mbegu kuota vizuri.
2. Njia nyingine ni kuotesha kwenye tuta lenye udongo wa kichanga na kisha kuhamishia mbegu kwenye viriba mara mbegu zinapotoa mzizi unaofikia sentimeta 2 hadi 3. Njia hii hutumika iwapo hukuna uhakika wa mbegu kuota vizuri.
3. Mwagilia maji kwenye viriba kabla ya kupanda au kuhamishia mbegu zilizowatikwa.
4. Fukua kishimo kidogo kisha panda mbegu kwenye kiriba huku kikonyo chake kikielekea juu kama inavyo kuwa kwenye bibo.
5. Funika juu ya viriba kwa nyasi kavu ili kuhifadhi unyevu na kuongeza joto.



*Upandaji wa mbegu kwenye kiriba*

**Utunzaji wa kitalu**

Viriba vimwagiliwe maji mara moja kwa siku, asubuhi au jioni. Hakikisha udongo kwenye viriba una unyevu wa wastani kila wakati.

Dhibiti mapema magugu, wadudu na magonjwa yanayoweza kujitokeza .

Miche itakuwa tayari kupandwa au kubebeshwa baada ya kuwa na majani 3 au zaidi.

## UTANGULIZI

Mikorosho inaweza kuoteshwa kwa kutumia mbegu moja kwa moja shambani au kuotesha kitaluni kwenye viriba na baadaye kuhamishia shambani. Kitalu cha mikorosho ni eneo linalotumika kuotesha na kutunza miche michanga ya mikorosho kabla ya kupandwa shambani.

Kipeperushi hiki kimeandaliwa ili kuwawezesha waoteshaji miche vitaluni na wakulima kuelewa taratibu zinazofuatwa katika uanzishaji wa kitalu.



### Faida za kitalu

1. Eneo dogo hututumika kuotesha na kuhudumia miche mingi
2. Hupunguza gharama za kuotesha na kutunza miche ikilinganishwa na gharama ambazo zingetumika kuhudumia shamba.
3. Ni rahisi kubaini na kudhibiti wadudu waharibifu na magonjwa.
4. Miche inayohamishiwa shambani huwa imefikia umri madhubuti wa kuweza kustahimili mazingira yasiyorafiki kwa ukuaji wa miche michanga mfano ukame' magonjwa, wadudu, na wanyama waharibifu.
5. Miche huweza kupangwa kwenye madaraja ya ubora, ambapo kila daraja linaweza kupandwa sehemu yake kwenye shamba. Miche dhaifu hutengwa kabisa.



### Sifa za eneo linalofaa kuanzisha kitalu – eneo liwe;

1. Karibu na maji yasiyo na chumvi, mengi na ya uhakika.
2. Linaloweza kufikika kirahisi.
3. Na mwinuko wa wastani kuepuka maji kutuama.
4. Liwe karibu na udongo unaofaa kujazwa kwenye viriba.

### Mahitaji kwa ajili ya kitalu

1. **Pembejeo**: Viriba, udongo wa msituni, samadi au mboji, mchanga (kama udongo sio wa kichanga), mbegu za korosho na vikonyo.
2. **Zana:** Visu, kamba za nailoni (tape), Jembe, panga, sepetu, reki, tolori, ndoo au keni ya kumwagilia maji.

### Jinsi ya kuandaa kitalu

1. Tengeneza/andaa sehemu ya kuwekea viriba iwe tambarare.
2. Kusanya pembejeo zote karibu na eneo la kitalu.
3. Tengeneza vivuli vya kuhifadhia miche.
4. Andaa mchanganyo wa udongo wa kuoteshea miche.

### Sifa za udongo unaofaa kuoteshea miche

1. Uwe tifutifu ili kuwezesha mizizi ya miche kupenya na kukua kirahisi, pia wenye kuhifadhi unyevunyevu wa kutosha kwa matumizi ya miche (Wenye asilimia 50 hadi 75 ya kichanga)
2. Uwe na virutubisho vya kutosha kukuzia mmea hadi utakapofikia wakati wa kupanda shambani. Ongeza mbolea ya NPK (5 – 10 g/lita) kama kichocheo cha virutubisho kwa ukuaji wa awali wa mche.

### Kutayarisha mchanganyo wa udongo wa kujaza kwenye viriba .

1. Chekecha mchanga na udongo au ondoa magugu, mawe na takataka kwenye udongo
2. Changanya udongo, mchanga na samadi/mboji kwa uwiano ufuatao – vipimo 2 vya udongo wa msituni + kipimo 1 cha mchanga + kipimo 1 cha mbolea ya samadi au mboji. (Kipimo kinaweza kuwa ndoo, debe, karai, sepetu ama tolori).
3. Changanya uwiano huu kwa sepetu/chepe huku ukinyunyizia maji kidogo kidogo kuufanya udongo uwe na unyevu bila kutengeneza tope au unao nata. Changanya viambato ipasavyo kuhakikisha vinachanganyika vinzuri mithili ya uchanganyaji zege,